



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA



OFISI YA MKURUGENZI WA MANISPAA  
HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA  
200 BR. YA BUSWELU  
33282 BUSWELU  
ILEMELA, MWANZA

Ijumaa, Tarehe 12 Agosti, 2022

**TAARIFA KWA UMMA**

**KUSITISHA MATUMIZI YA KITUO CHA MABASI CHA BUZURUGA NA  
SHUGHULI ZOTE ZA USAFIRI WA MABASI KUHAMIA STENDI MPYA  
YA NYAMHONGOLO**

Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela imetekeleza mradi wa kimkakati wa ujenzi wa kituo kipyaa cha Mabasi cha kisasa katika eneo la Nyamhongolo, hivyo kufuatia kukamilika kwa mradi huo imelazimu kusitisha matumizi ya kituo cha mabasi cha Buzuruga na shughuli zote za usafiri wa mabasi kuhamia Nyamhongolo kuanzia **Jumane, Tarehe 16 Agosti, 2022.**

Wapangaji wote wa Halmashauri wenye biashara za mabasi (usafirishaji wa abiria) na wenye ofisi za kukatia tiketi katika stendi ya mabasi Buzuruga wanajulishwa kuwa Halmashauri itawapatia vyumba vya kukatia tiketi katika kituo cha mabasi Nyamhongolo ambacho wataanza kutumia kuanzia **Jumane, tarehe 16 Agosti, 2022**

Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela, S.L.P 735, Mwanza.

BaruaPepe:md@ilemelamc.go.tz, Tovuti: www.ilemelamc.go.tz

Page 1

Hivyo wananchi wote mnajulishwa kuwa, shughuli zote za usafiri katika stendi ya mabasi Buzuruga zitasitishwa siku ya **Jumane Tarehe 16 Agosti, 2022** na shughuli hizo kuhamia Stendi mpya ya mabasi ya Nyamhongolo.

**IMETOLEWA NA:**



**ENG. MODEST J. APOLINARY**  
**MKURUGENZI WA HALMASHAURI**  
**MANISPAA YA ILEMELA**



*Jiandae Kuhesabiwa siku ya Jumane tarehe 23 Agosti, 2022*